## 4.0 KISWAHILI

Uchanganuzi wa matokeo ya mwaka wa 2008 umefanywa kwa kulinganishwa na yale ya miaka ya **2005, 2006** na **2007**.

**Fahirisi 8: Matokeo ya Kiswahili KCPE ya miaka ya 2005 hadi 2008**

| | 2005 | | 2006 | | 2007 | | 2008 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** | **Lugha** | **Insha** |
| | **50** | **40** | **50** | **40** | **50** | **40** | **50** | **40** |
| Alama ya wastani | 30.3 | 18.06 | 29.89 | 18.32 | 25.51 | 16.99 | 28.30 | 18.40 |
| Alama iliyotuzwa Watahiniwa wengi | 32 | 20 | 33 | 18 | 26 | 16 | 30 | 18 |
| Alama ya juu iliyotuzwa | 50 | 39 | 50 | 39 | 49 | 39 | 50 | 40 |

Fahirisi hii inatuonyesha kuwa kwa upande wa lugha:

(i) Alama ya wastani imepanda kutoka alama **25.51** mwaka wa **2007** hadi **28.30** mwaka wa **2008**.

(ii) Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi pia imepanda mpaka **30** mwaka wa **2008** kutoka **26** mwaka wa **2007**.

(iii) Alama ya juu iliyotuzwa imepanda kwa alama moja kutoka **49** mwaka wa **2007** hadi **50** mwaka wa **2008**.

Kwa upande wa insha:

(i) Alama ya wastani imepanda kutoka alama **16.99** mwaka wa **2007** hadi **18.40** mwaka wa **2008**.

(ii) Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi imepanda kutoka alama **16** mwaka wa **2007** hadi **18** mwaka wa **2008**.

(iii) Alama ya juu iliyotuzwa imepanda kutoka **39** mwaka wa **2007** hadi **40** mwaka wa **2008**.

POWERED BY: WWW.MANYAMFRANCHISE.COM

Mchoro huu unatuonyesha vile alama za sehemu za lugha na insha zilivyojitawanya.




Figure 3 - Kiswahili

Mchoro huu unatuonyesha ijapokuwa watahiniwa wengi waliweza kupata alama nusu ya alama zote zinazoweza kutuzwa katika upande wa lugha, **(25/50)**, Katika insha watahiniwa wengi hawakufikia nusu ya alama zote zinazoweza kutuzwa **(20/40)**.

## 4.1 SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

Mchoro huu unatuonyesha asilimia ya watahiniwa tuliochanganua ambao walipata jibu sawa katika kila swali.




Figure 4 - Kiswahili Lugha

Kila mwaka huwa tunachanganua maswali ambayo yaliwatatiza watahiniwa. Mwaka wa **2008** maswali ambayo yalionekana kuwatatiza watahiniwa ni swali la **20, 26, 43** na **50**. Haya ni maswali ambayo chini ya watahiniwa asilimia thelathini **(30%)** ya wale tuliochanganua waliweza kupata jibu sawa.

**FAHIRISI YA 9: Maswali ambayo yaliwatatiza watahiniwa**

| **Maswali** | **20** | **26** | **43** | **50** |
|---|---|---|---|---|
| Asilimia ya watahiniwa waliopata jibu sawa | 24.24 | 28.01 | 19.08 | 29.91 |
| Alama ya wastani ya maswali yale mengine | 34.35 | 32.51 | 33.98 | 31.16 |

**Swali la 20:**

*Kutoka swali la* **16** *mpaka* **30**, *chagua jibu lililo sahihi.*

Methali yenye maana sawa na "usiache mbachao kwa msala upitao" ni
A. usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi
B. bahati ya mwenzio usiilalie mlango wazi
C. usipoziba ufa utajenga ukuta
D. bura yangu siibadili na rehani.

**Matokeo ya swali la 20**

| **Majibu** | **A** | **B** | **C** | **D*** |
|---|---|---|---|---|
| % ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 40.59 | 19.61 | 14.73 | 24.24 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine. | 29.81 | 27.54 | 27.60 | 34.35 |

*Inaonyesha Jibu sawa.

Swali hili lilikuwa la matumizi ya methali. Mtahiniwa alitakikana awe anajua maana ya methali ***"Usiache Mbachao kwa msala upitao"***, ndipo aweze kuchagua methali nyingine iliyo na maana sawa.

Methali hii inamaanisha mtu asiache kile kilicho chake ama alicho nacho, kwa kutaka kingine ambacho si chake na pengine huenda asikipate. Ni methali ambayo inaonyesha mtu kumiliki kitu kati ya nne zilizotolewa **D** ***(bura yangu siibadili na rehani)***. Jibu la **A** (***usione kwenda mbele kurudi nyuma si kazi)*** linaonya dhidi ya mtu kujitapa na kuona kwamba pengine yuko bora kwa cheo kwa mfano, kuliko watu wengine. Jibu la **B** ***(bahati ya mwenzio usiilalie mlango wazi)*** vile vile laonya dhidi ya kufikiria kwamba kwa sababu mwenzako amebahatika kwa aina fulani, nawe waweza kubahatika hivyohivyo. Jibu la **C** ***(usipoziba ufa utajenga ukuta)*** lahimiza mtu kutatua mambo au matatizo madogo yanapozuka yasije yakawa makubwa zaidi yakamshinda.

**Swali la 26:**

Ugonjwa wa **ukambi** pia huitwa

A. surua
B. safura
C. ndui
D. tetewanga

**Matokeo ya swali la 26**

| Majibu | A* | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| % ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 28.01 | 21.97 | 19.27 | 29.76 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine. | 32.51 | 28.75 | 29.45 | 29.38 |

*Inaonyesha jibu sawa.

Swala hili lilikuwa la mbinu ya ujuzi.

Kutokana na vile watahiniwa wanavyojitawanya katika majibu yao, inaonekana wengi hawakujua jibu kabisa wakabaki kubahatisha tu. ***Safura*** ni ukosefu wa damu mwilini, ***ndui*** ni vipele vyenye usaha nao ***tetewanga*** ni homa kali inayoambukiza watoto. Jibu la swala hili lilikuwa **A.** ***(Surua).***

*Soma taarifa hii kisha ujibu maswali **41** mpaka **50**.*

Wanafunzi wa shule ya Mtepetevu walitembelewa na wazazi. Kabla ya kuruhusiwa kukutana na watoto wao, wazazi waliingia kwenye mkutano. Takriban kila mzazi alimbebea mwanawe furushi la chakula, licha ya kuwa watoto wao walikuwa wamerudi kutoka nyumbani majuma mawili tu yaliyopita.

Mkutanoni wazazi walizozana kuhusu maakuli shuleni, mavazi na mitindo ya nywele ya watoto hao. Baadhi walitaka watoto wao wapewe mapochopocho na matunda ghalighali. Wengine wao siku hiyo hawakufikiria sana kuhusu juhudi za watoto masomoni, kinyume na kawaida yao. Hata hivyo, wengi wao waliona mbele, wakapinga udekezaji huo.

Mzozo ulipokuwa <u>ukipamba moto</u>, kijana mmoja wa karibu miaka ishirini na minne, aliyekuwa amevalia kilalahoi, akaingia mkutanoni. Baadhi ya wazazi waliomuona walishindwa kwani mkutano ulikuwa ni wa wazazi. Kijana akaketi na kutega sikio. Mzazi mmoja alisimama na kusema, "Nimeitazama orodha hii ya vyakula na nimesikitika. Kwa nini hawa watoto hawapewi chapati kwa kima, pilau na 'matoke'? Tunalipa! Sasa kwa nini wanakula ugali na '*githeri*'".

Kijana yule alikereketwa, akaunyoosha mkono juu sana na alipoona anapuuzwa, akasimama na kuanza kusema, "Hoja mnazotoa si ...." Baadhi ya wazazi wakamdakia na kusema, "We! Nyamaza. U mtoto! U mkwe wetu...". Kijana akazidi kukakawana na kutaka kupewa nafasi lakini wale waliokuwa karibu naye wakamlazimisha kuketi. Mwenyekiti akasema, "Huu ni mkutano wa wazazi. Jukumu lako kijana ni kunyamaza na kusikiliza kwa makini, kisha uwapelekee wazazi ujumbe."

Kijana alikazana, "Tafadhali nipeni ruhusa. <u>Kitanda msichokilalia, hamuwajui kunguni wake</u>." Akaulizwa walikokuwa wazazi wake kwani ndio waliotakiwa mkutanoni. Akajibu, "Bwana Mwenyekiti, sina wazazi! Mimi ni mlezi wa wadogo zangu, nina mdogo wangu hapa. Nimetoka mbali huko kote kuja kuwawakilisha marehemu wazazi wangu. Mimi si mlevi, si mhuni au mkwe wenu. Nina akili razini. Kuwa kijana si dhambi. Nimemaliza chuo kikuu. Nina kazi lakini mshahara wote unaishia kwenye malezi na sasa mnanikataza kusema lolote. Je, kijana hana haki? Ninajua kuwa maji mengi hayazuiliki lakini tushirikianeni kwani penye wengi hapaharibiki neno".

Mwenyekiti akampa nafasi ya kujieleza. Kijana akaendelea, "Mimi kama kijana mlezi, nimewasikiliza kwa makini. Ninapinga hoja ya mavazi ya nyumbani na mapochopocho kama chapati....Jambo linalofaa ni kuwafunza kutafuta elimu kwa bidii. Wakihimizwa kuwa na adabu na kuwa na kiu ya masomo, watajikataza wenyewe kufuata tu raha maishani. Kula bila kujua kutafuta kutawatia mashimoni. Mvumilivu hula mbivu. Kugeuza mandhari ya shule kuwa ni sehemu ya mandari kutajenga uvivu, wizi, matabaka na wivu shuleni. Wanafunzi watawabeza walimu, badala ya kuwasikiliza. Tuwafunze kujitegemea". Wazazi walimhurumia na kumpigia makofi. Mwenyekiti akamuomba msamaha na kumshukuru kwa niaba ya wazazi.

**Swali la 43:**

Mkutanoni kulikuwa na:
A. wapinzani, mwenyekiti na kijana
B. waungaji mkono, kijana na mwenyekiti
C. wageni, kijana na mwenyekiti
D. wadekezaji, waona mbele na mwenyekiti

**Matokeo ya swali la 43**

| **Majibu** | **A** | **B** | **C** | **D*** |
|---|---|---|---|---|
| % ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 41.24 | 18.63 | 19.99 | 19.08 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine. | 30.04 | 28.80 | 27.94 | 33.98 |

*inaonyesha jibu sawa.

Swali hili lilikuwa latahini mbinu ya usanisi ambapo mtahiniwa anakusanya mambo tofauti yakawa jibu. Jibu la **A** ***(wapinzani, mwenyekiti na kijana)*** lilivutia watahiniwa wengi. Lakini tukiangalia kifungu tunaona kwamba hapakuwa na mjadala ambapo mtu angeunga jambo hili au lile mkono. Swala la kuwa na wapinzani au waunga mkono halingeshuka.

Baadhi ya wazazi kuna wale, pamoja na kijana walikuwa hawapendelei udekezaji wa watoto. Hawa wote ni waona mbele. Wazazi wengine walikuwa ni wadekezaji. Naye mwenyekiti alikuwa pale kuongoza kikao. Kwa hivyo jibu sahihi lilikuwa **D** ***(Wadekezaji, waona mbele na mwenyekiti)***.

**Swali la 50:**

Kichwa mwafaka kinachofaa kuelezea taarifa hii ni:
A. Dhifa ya wazazi shuleni.
B. Ujana shuleni si hoja.
C. Mzozo na mapatano shuleni.
D. Kudunishwa kwa vijana shuleni.

**Matokeo ya Swali la 50**

| **Majibu** | **A** | **B** | **C*** | **D** |
|---|---|---|---|---|
| % ya watahiniwa waliochagua jibu hili | 41.43 | 10.51 | 29.91 | 17.28 |
| Alama yao ya wastani ya maswali yale mengine. | 30.87 | 27.17 | 31.16 | 28.44 |

* Inaonyesha jibu sawa.

Swali hili lilitahini mbinu ya tathmini. Jibu la A ***(dhifa ya wazazi shuleni)*** lilivutia wengi. Kifungu hiki hakizungumzii dhifa ya wazazi moja kwa moja. Kile tunachoona ni kwamba wazazi wanafika shuleni na waingiapo mkutanoni mabishano yanaanza na kuendelea mpaka pale kijana anapoonekana kutoa mwongozo unaokubalika na wote. Hapo wanaonekana kupatana. Kwa hivyo jibu sahihi ni **C**. ***(Mzozo na mapatano shuleni)***.

## 4.2 SEHEMU YA PILI: INSHA

Mwaka wa **2008** insha ilikuwa

Andika insha isiyopungua ukurasa mmoja na nusu juu ya kichwa kifuatacho:

Anza kwa: Wingu kubwa jeusi lilitokea upande wa mashariki. Baadaye matone mazito mazito ......

Katika Insha hii mtahiniwa amepewa kichwa ambacho kinamwelekeza kuweza kuandika insha yake kwa njia anayotaka mwenyewe.

Yafuatayo ni maelezo kuonyesha jinsi alama katika viwango vinne maalum zinavyofikiwa katika usahihishaji. Viwango hivi ni vya alama **01-10, 11-20, 21-30, 31-40.**

### 4.2.1 Kundi la kwanza (alama 01-10)

Watahiniwa hawa, hasa wale waliotuzwa alama **01-05**, huwa wameandika insha zao vibaya mno. Baadhi yao hutumia maneno ya Kiswahili, kiingereza na hata lugha zao za mama kiholela tu bila kuunda sentensi yoyote. Wale waliotuzwa alama **6 – 10** huwa wameandika insha zao kwa Kiswahili kilicho na makosa mengi sana ya sarufi na tahajia. Mawazo yao hayatokei vizuri. Huwa pia wamepotoka kwa upande wa mada.

**Mtungo wa Kwanza**

Anza kwa: Wingu kubwa jeusi lilitokea upande wa mashariki. Baadaye matone mazito mazito ......

Anazai sai cis waza lisulthe whzi samzi keie wde
kei sam wdaieige ig e, peie kaigel baadaye forosuiezit
Fatzie wde izuidea dlezn tonezei kei wdidam damigar
damza wdeie mazioe mazito abiz keigundi
inize peitomi maziwtam dam whezaimigamsa
kwa maingu kubwa jeusi lilitoke dim dam dei
fkeza uzmaige famde mazawde ditomde wde wamde
kamzei maziwnizc gamdzeiew dei melond mazi
ito kubwa jeusi litokea upande wa masnarikei dumzu
meazi tamzeike mataeom ewde dam zamei izi zaie
famwa damde wde sam damde wda wde dawdeie
udigozi poizie wdu semealda wdedumde samie su
damige ziemcum damde wdc dam de wde ded
pampam ewdei wdei dumze zlewdu damde